
Ghorofa ya 7, Jengo la LAPF Pension Fund, Mkabala na Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama
S.L.P. 72175, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255-022 2923513-18; Nukushi: +255-22 2923519
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TAARIFA KWA UMMA

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inapenda kuwatangazia waombaji wote wa leseni na vibali vya ujenzi katika Sekta ndogo ya mafuta ya petroli, mkondo wa kati na chini kwamba; kuanzia tarehe **5/4/2018**, maombi ya leseni na vibali vya ujenzi yanatakiwa kufanyika kwa njia ya mtandao unaoitwa *Licensing and Order Information* (LOIS) kupitia anuani ifuatayo: <https://lois.ewura.go.tz>. Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya EWURA www.ewura.go.tz.

Lengo la kutumia njia ya mtandao kutuma maombi ya leseni ni kupunguza muda wa upatikanaji wa leseni zinazotolewa na EWURA na pia kuwawezesha waombaji kupata taarifa za maombi yao moja kwa moja katika mfumo huu.

Kwa maelezo zaidi, unaweza kutembelea ofisi zetu zilizoko Dodoma (Makao Makuu-Jengo la LAPF, GHOROFA YA 4) na Ofisi za Kanda zilizoko Arusha, Dar es Salaam, Mbeya na Mwanza.

IMETOLEWA NA:

KAIMU MKURUGENZI MKUU

EWURA